**Learning By Ear 2011 Biashara – "Kuanzisha Biashara"**
**Kipindi cha 8: "Kufadhili"**
AUTHOR: Erick-Hector HOUNKPE
EDITORS: Yann Durand, Aude Gensbittel
TRANSLATOR: Anne Thomas
PROOFREADER: Charlotte Collins

## Characters

Msimulizi

Daniel Huba (Mwanamume, umri wa miaka 29)

**Scene 1:**

**KOSSI:** (Mwanamume, umri wa miaka 18)

**ABBAS:** (Mwanamume, umri wa miaka 21)

**MARIAM:** (Mwanamke, umri wa miaka 19)

**KOSSI'S FATHER:** (Mwanamume, umri wa miaka 55)

**LINDA:** (Mwanamke, umri wa miaka 20, dadake Kossi)

**Scene 2:**

**KOSSI:** (Mwanamume, umri wa miaka 18)

**ABBAS:** (Mwanamume, umri wa miaka 21)

**THE SECRETARY:** (Mwanamke, umri wa miaka 25)

**CUSTOMER:** (Mwanamume, umri wa miaka 45)

**BANKER:** (Mwanamume, umri wa miaka 50)

**Scene 3:**

**KOSSI:** (Mwanamume, umri wa miaka 18)

**ABBAS:** (Mwanamume, umri wa miaka 21)

**MARIAM:** (Mwanamke, umri wa miaka19)

**MR. MASINGA:** (Mwanamume, umri wa miaka 57)

**Learning By Ear 2011 Biashara – "Kuanzisha Biashara"**
**Kipindi cha 8: "Kufadhili"**
AUTHOR: Erick-Hector HOUNKPE
EDITORS: Yann Durand, Aude Gensbittel
TRANSLATOR: Anne Thomas
PROOFREADER: Charlotte Collins

## INTRO

### Host:

Hamjambo na karibuni kwenye Noa Bongo Jenga Maisha Yako na kipindi kingine katika mfululizo wa vipindi vyetu kuhusu kuanzisha biashara. Mpaka sasa, wajasiriamali wetu vijana Mariam, Abbas na Kossi wameanzisha kampuni yao ya usanifu wa ndani na usimamizi wa matamasha iitwayo Young Design. Katika kipindi kilichopita walitathmini bajeti yao na pia wakatenga ada watakazotoza kwa huduma zao. Lakini watatoa fedha wapi? Kipindi hiki cha nane kinahusu "Ufadhili" na kinaanza kwa ushauri wa mtaalamu wetu, Daniel Huba, mhadhiri wa Kituo cha Kieneo cha Ustawi wa Ujasiriamali katika Chuo Kikuu cha Inorero nchini Kenya.

### 1. Daniel Huba 45''

*Ebu tuangalie namna za kufadhili biashara yako. Jinsi moja ya kufadhili biashara yako ni akiba yako binafsi. Pengine umetundiza fedha kidogo kidogo kwa muda na unataka kuzitumia fedha hizo kuanzisha biashara yako. Hizi fedha hazikutatizi sana, maana ni zako. Hutamlipa mtu wala hutakiwi kulipa riba. Lakini wakati mwingine huna fedha za kutosha kuanzisha biashara. Hata hivyo ni muhimu kukumbuka ukiwa mfanyabiashara ni vyema kujiwekea akiba. Usijizoeze kutegemea unachopewa. Namna ya pili ya kupata mtaji ni kutegemea marafiki na jamaa zako. Marafiki na jamaa zako wanaweza kukukopesha fedha. Ama bila riba yoyote- maanake huhitajiki kulipa mkopo huo kwa riba, uanze biashara yako na pindi upatapo fedha uwalipe deni lao. Wengine watasema, hii ni biashara, kwa hivyo tutakudai kiasi kidogo. Kwa hivyo inategemea na makubaliano yako na wao.*

AUTHOR: Erick-Hector HOUNKPE
EDITORS: Yann Durand, Aude Gensbittel
TRANSLATOR: Anne Thomas
PROOFREADER: Charlotte Collins

2. **Narrator:** Abbas, Kossi na Mariam wamejiwekea fedha kidogo. Lakini hata wanapojumuisha hizo fedha, si kiasi kikubwa– wala si kiasi kinachotosha kuwa mtaji wa kuanzisha kampuni yao. Kwa hivyo wameamua kuwaomba msaada jamaa na marafiki zao.

**<u>Scene 1: At Kossi’s house</u>**

**Linda, Mariam, Kossi’s dad, Abbas, Kossi**

| |
|---|
| 3. **ATMO : Outside, leaves rustling, barking, hens** |

4. **LINDA**: (**Worried**) Nina wasiwasi kidogo, Mariam. Hivi karibuni baba yetu namwona amekuwa siye yule tumjuaye. Hata mama anashindwa kumdhibiti …

5. **MARIAM:** Tuombe Mungu, Linda. Alisema atatusaidia, na nina hakika ndugu yangu atajaribu kumshawishi!

6. **KOSSI’S DAD**: **(From a distance, angrily)** Sikiza, acha kunisumbua! **(getting closer and louder)** Wewe na dadako mnayajua matatizo ambayo nimekuwa nikikabiliwa nayo kiasi miezi mitatu iliyopita.

7. **ABBAS AND MARIAM:** Shikamoo, mzee!

8. **KOSSI’S DAD:** Marahaba, wanangu. Ketini, tafadhali.

| |
|---|
| 9. **SFX: Sound of chairs** |

10. **KOSSI'S DAD:** **(clearing his throat as if he's looking for the right words)** Wanangu, najua niliwaahidi kwamba nitawasaidia … lakini uwezekezaji huu wote, miradi ya kupata fedha kwa haraka … huenda ukafikiri kwamba utapata faida haraka iwezekanavyo unapowekeza kwenye jambo fulani, kisha unakumbana na matapeli ambao wanakimbia na akiba yako yote. Hata kama una uzoefu mkubwa kiasi gani, unaishia kufanya kosa hilo hilo. Nasikitika kusema kwamba nimelaghaiwa fedha nyingi sana kwa njia hii. **(In a more reassuring tone)** Lakini ninakuhakikishieni, pindi hali yangu ya kifedha ikitengemaa, ninaahidi sitawasahau … Ninawatakia kila la heri!

11. **SFX: Steps going away (1 person)**

12. **The young people**: Asante sana…

13. **KOSSI:** **(Sad and disappointed)** Samahani sana…

14. **MARIAM**: Si kosa lako, Kossi…

15. **ABBAS:** Wala tusikate tama. Babako ametuahidi kwamba atatusaidia– ni kwamba msaada wenyewe utachukua muda mrefu kuliko tulivyotarajia.

**16. MARIAM:** Sasa hivi tunatakikana kushughulisha sana akili zetu. Ebu tuiangazie tena orodha ya wafadhili wetu.

| **17. SFX: Rustling of paper** |
|---|

**18. KOSSI**: Naam, Mariam, wazazi wako, walitupatia dola 100, na wakatukopesha kiasi kingine kama hicho cha fedha.

**19. MARIAM**: Hizo tutalipa baadaye. Na mwingine?

**20. KOSSI**: Wazazi wake Abbas walitupatia kiasi fulani cha fedha– dola 50 – na marafiki zetu wacheza kamari wamekusanya dola 40, kama vile marafiki zetu wa zamani shuleni. Abbas, shangazi yako aliyeko Paris ametuletea hundi ya dola 300. Na zaidi tuna akiba ya dola 145. John na Linda wametuchangia dola 80 … Nadhani ni hayo tu…

**21. ABBAS**: Kwa jumla ni pesa ngapi?

**22. KOSSI**: (**Slowly**) Kwaaa… jumlaaa…

| **23. SFX: Calculator buttons being pressed** |
|---|

**24. KOSSI:** **(talking to himself)** 50 kuongeza 40 na hii ….ahhhm…. **(loudly)** Kwa jumla tuna dola 615.

**25. MARIAM**: Umm… Tunahitaji dola 1000 za mtaji wa kuanzia. (**silence again**) Kwa hivyo tulizo nazo hazitoshi.

**26. LINDA**: Jamani, tusikate tama. Ni lazima tujikaze. Tazama hiyo orodha, Kossi, utueleze watu wangapi walioahidi kutusaidia kwa fedha na bado hawajatimiza ahadi zao.

**27. KOSSI**: SAWA. **(Pause)** 1..2..3, 4, 5..6 eee, naam, watu sita.

**28. ABBAS**: Tujaribu tena kuwaomba. Huenda baadhi yao wakatufaa.

**29. Narrator:** Jamaa na marafiki wana nia njema lakini hawawezi kumfaa mtu kifedha ikiwa hawana uwezo huo. Wajasiriamali hawa wachukue hatua gani nyingine, endapo hawatapata fedha za kutosha hata baada ya kuomba msaada wa jamaa na marafiki zao? Mtaalamu wetu Daniel Huba ana ufumbuzi wa tatizo hilo:

**30. Daniel Huba 49’’**

*Namna ya tatu ni kupitia benki. Lakini ni muhimu kutambua kwamba unapotaka fedha kutoka benki, ni lazima uandae nyaraka kadha. Huo unaitwa mpango wa biashara. Inakubidi uiandike aina ya biashara yako na kiasi itakachokugharimu. Na wataamua ama kukufadhili au kutokufadhili kulingana na maandishi yako hayo. Au mwisho, unaweza kuzingatia mchanganyiko. Mathalan, unaweza kusema, biashara yangu inagharimu dola 500, na mimi nina dola 200. Ikiwa mimi ni kijana, je kuna hazina ya vijana nchini? Kisha*

*unawaendea wanaohusika na hazina hiyo unawaambia: 'Jamani, mimi nina dola 200, mnaweza kuniongezea dola 300?' Kwa kawaida utasaidiwa maana tayari umejiwekea akiba fulani. Au unapokwenda kwenye benki. Unaweza kuchanganya akiba yako binafsi na mkopo kutoka ama taasisi ya kifedha, hazina maalumu au benki. Kwa hivyo wewe ndiye unayeamua taasisi gani ya kuchagua.*

**31. Narrator:** Wajasiriamali wetu vijana wanafikira kuchukua mkopo kuongezea kiasi cha fedha ambazo tayari wamekusanya. Wanakwenda benki kujua masharti, lakini wanakumbana na mambo wasiyotarajia …

## Scene 2 : At the bank

**Abbas, Kossi, Mariam, Secretary, Client, Banker**

| |
|---|
| **32. ATMO: Inside, bank, computer keyboards, printers** |

**33. ABBAS:** Nenda, Kossi. Shubaka la taarifa lile pale. Wewe ndiye unayeweza kujieleza vizuri, kwa hivyo mimi na Mariam tutakusubiri hapa.

| |
|---|
| **34. SFX: Sound of steps (1 person)** |

**35. KOSSI**: Hujambo. Nimekuja kupata taarifa fulani …

AUTHOR: Erick-Hector HOUNKPE
EDITORS: Yann Durand, Aude Gensbittel
TRANSLATOR: Anne Thomas
PROOFREADER: Charlotte Collins

**36. THE SECRETARY:** **(In a friendly tone)** Keti, tafadhali… nipe dakika moja kwa hisani yako … nimalize ninalofanya kisha nitakushughulikia …

**37. SFX: Person sits down on a chair**

**38. SFX: Sound of computer keyboard**

**39. CUSTOMER**: **(a bit further away, speaking loudly)** Una maana gani? Usiseme hivyo. Nakwambia nimetatizika kwa kiasi kikubwa! Ninachotaka ni hiyo tarehe kusogezwa mbele ili niweze kulipa mkopo, na benki, benki YANGU inakataa…

***The dialogue between the CUSTOMER and the BANKER continues while the secretary is talking***

**40. THE SECRETARY**: **(sighing)** Jamani – mwingine huyo anayekabiliana na hali ngumu …

**41. BANKER**: Tafadhali. Tulia, tafadhali!

**42. CUSTOMER**: Mnasema mnataka kuichukua nyumba yangu, ingawa ninalipa kidogo kidogo! Mnanidai elfu15, na mnataka kutwaa nyumba yangu ya thamani ya 50,000… na si kwamba biashara yangu ndio mbaya – mnajua vyema mkasa wa moto ulionipata. Nyinyi ni waovu kweli!

**43. BANKER**: Sikiza, kwa hisani yako, tuko kwenye benki. Tafadhali punguza sauti yako. Ulishatia saini. Ndivyo sheria ilivyo. Kuna vifungu kwenye mkataba vinavyoeleza mambo yanavyokuwa katika hali kama hii.

**44. CUSTOMER**: Vifungu gani? Ati vifungu! Nyinyi nyote ni matapeli! Lakini hamtaniwahi! Nakwambia kweli, hamtaniwahi! (**He walks away shouting**) Nitawajulisha mawakili wangu. Nitapambana nanyi vilivyo, mtaniona …

**45. THE SECRETARY:** **(To Kossi)** Ninakusikiliza. Samahani kwa zogo hilo. Nikusaidie nini?

**46. KOSSI:** **(Shocked by the scene)** Eee, um, hapana, samahani mama, nili… ee…

**47. SFX: Chair pulled back, person leaves**

**48. KOSSI**: **(A bit more loudly)** Nilitaka kujua tu taratibu za kufungua akaunti… lakini nadhani nitakuja wakati mwingine.

**49. THE SECRETARY:** **(from a distance)** HAYA! Uwe na siku njema! Karibu tena!

**50. KOSSI**: **(To Mariam and Abbas)** Nimeogopa mimi. Ikiwa mtu anaweza kupoteza kilicho chake vivi hivi tu sidhani kama tuna haja ya kuchukua mkopo. Twendeni zetu!

AUTHOR: Erick-Hector HOUNKPE
EDITORS: Yann Durand, Aude Gensbittel
TRANSLATOR: Anne Thomas
PROOFREADER: Charlotte Collins

## Scene 3: At Mr. Masinga's on the terrace

**Mr. Masinga, Kossi, Mariam, Abbas**

**51. ATMO: Outside in the daytime, sound of leaves rustling, birdsong, traffic in the distance…**

**SFX: Sound of glasses and drinks being poured**

**52. MR. MASINGA**: (**Calm and optimistically**) Changamkeni, wanangu. Msisikitike. Wala haya yasiwavunje moyo.

**53. KOSSI**: (**Down**) Wajua, Mjomba, tuliyoyaona kwenye benki yametuchanganya.

**54. MR. MASINGA**: Ni kweli kwamba maisha si rahisi. Vya bwerere ni nadra kupatikana. Hata hivyo mnapaswa kushukuru Mungu kwamba baadhi ya jamaa na marafiki zenu wanawasaidia ingawa na wao wana shida zao pia. Kwenye hicho kiasi cha 1000 mnachohitaji, nyinyi wenyewe mmefaulu kukusanya kiasi gani?

**55. ABBAS**: Dola 615.

**56. MR. MASINGA**: SAWA, naam, mnapaswa kujua kwamba si rahisi kupata mtaji– ni tatizo la kawaida. Nilikuwa na tatizo lilo hilo nilipokuwa nikianzisha kampuni yangu. Lakini nilipata fedha. Nilibahatika kumpata "malaika wa biashara".

**57. KOSSI**: Malaika wa biashara ndiye nani?

58. **MR. MASINGA**: Naam, kimsingi ni mtu anayewekeza kwenye mradi wa kujaribisha ambao anadhani una dalili za ukafaulu kwa kiasi kikubwa. Si fedha tu wanazowekeza bali pia huwasaidia wajasiriamali wachanga kwa kuwapa ujuzi, rasilimali na pia huwasiliana nao mara kwa mara..

59. **ABBAS**: (**Happy**) Mashaallah ! Je watu kama hao wangalipo? Vipi mtu anaweza kumpata mmoja wao?

60. **MR. MASINGA**: Naam, wanagalipo. Lengo lao ni kuwasaidia wajasiriamali vijana kuzindua vyema biashara zao, na inawabidi nao wajikakamue vilivyo. Lakini hao "malaika wa biashara" pia wanatumai kwamba biashara itaimarika na watafaidika na uwekezaji huo.

61. **MARIAM**: (**Enthusiastically**) Unaweza kutupatia anwani kadha kwa hisani yako?

62. **MR. MASINGA**: **(laughing)** Sivyo mambo yalivyo … **(More seriously)** Lakini wanangu, ninaweza kuwa "malaika" wenu. (**Silence**)

63. **ABBAS**: (**Completely shocked**) Samahani? – Kweli? Unataka kuwa "malaika" wetu wa biashara!?

64. **MR. MASINGA**: Niachieni mpango wenu wa biashara, na taarifa yenu ya fedha, ili niuchunguze mradi wenu kwa kina

65. **KOSSI**: Siamini ninayosikia!

**66. MR. MASINGA**: Naam, nikiwasaidia, ninasaidia kuimarisha mtandao wa wajasiriamali wazuri humu nchini na hivyo kusaidia uchumi wa nchi yetu. Na ninawafanyia haya leo ila nyanyi muwafanyie wengine kesho, pindi mkianza kujisimamia, na mchakato mzima huo utaendelea hivyo. Kumbukeni, binadamu ni kufaana…

**67. ABBAS**: Kweli wewe ni malaika.

**68. Altogether**: Asante sana, Mjomba Masinga.

**69. MR. MASINGA**: Tutaonana karibuni, wanangu. Lakini ninawatahadharisha – nina sharti moja …!

**<u>OUTRO:</u>**

**Host:**

Na huo ndio mwisho wa kipindi cha nane cha mfululizo wa vipindi vyetu vya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu kuanzisha biashara, vinavyomhusisha . Baada ya kukabiliwa na matatizo chungu nzima wakati wakikusanya fedha, marafiki zetu hatimaye wameangukiwa na nyota ya jaha. Lakini masharti gani ambayo Bwana Masinga atawapa? Jiunge nasi katika kipindi kitakachofuata kwa mengi zaidi.

Ukitaka kusikiliza kipindi hiki tena au vipindi vingine vya Noa Bongo Jenga Maisha Yako tazama wavuti wetu www.dw.de/kiswahili. Hapo pia utapata taarifa zaidi kuhusu jinsi ya kuwa mjasiriamali. Kwa heri kwa sasa na usikose kujiunga nasi kwenye kipindi kinachofuata!

**END**